

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 FEBRUARI, 2018) NA MATARAJIO YA MVUA KWA SIKU KUMI (11– 20 FEBRUARI, 2018)

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 FEBRUARI, 2018)

Katika siku kumi za mwanzo za mwezi Februari 2018, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo Kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo wakati ile iliyopo sehemu ya Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika kidogo na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kubaki Tanzania hususani katika meneo ya nyanda juu Kusini-Magharibi pamoja na maeneo ya kusini mwa nchi, hali hii ilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua kubwa katika maeneo hayo. Joto la Bahari katika Bahari ya Hindi ilikuwa ya wastani hivyo kusababisha upungufu wa mvua maeneo ya Pwani na ukanda wa kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine kumekuepo na joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) hali iliyosababisha kupungua kwa vipindi vya mvua katika ukanda wa Ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 FEBRUARI, 2018)

Mwenendo wa viashiria vya hali ya hewa hapo juu ulipelekea vipindi kadhaa vya mvua zilizoambatana na radi katika maeneo ya nyanda za juu Kusini-Magharibi na mkoa wa Ruvuma, vipindi vichache vya mvua zilizoambatana na radi katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi, wakati maeneo ya ukanda wa Pwani ya Kusini na kanda ya kati vilikua na vipindi vichache vya mvua.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KATIKA SIKU KUMI (11–20 FEBRUARI, 2018)

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI (11–20 FEBRUARI, 2018)

Katika kipindi cha siku kumi za kati za mwezi Februari, migandamizo mikubwa iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuimarika kidogo wakati migandamizo mikubwa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kudhoofika kidogo. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kushuka kidogo kuelekea kusini na kubaki katika meneo ya Kusini zaidi mwa nchi, hali hii itapelekea kuwepo kwa upungufu wa vipindi vya mvua katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kutokea kaskazini mashariki na hivyo vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani, hususani katika ukanda wa Pwani ya Kusini. Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwepo kwa joto la juu kidogo ya wastani hadi juu ya wastani na hivyo upepo kuvuma kutoka mashariki na kuchangia upungufu wa mvua katika ukanda wa Ziwa Viktoria na Magharibi mwa nchi.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA SIKU KUMI (11–10 FEBUARI, 2018)

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Vipindi vichache vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Makavu kwa ujumla na vipindi vya jua.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja navisiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vichache vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Makavu kwa ujumla na vipindi vya jua.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya): Vipindi vichache vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Vipindi kadhaa vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Imetolewana; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**